OFISI YA RAIS -- TAMISEMI
SHULE YA SEKONDARI IPELELE

SHULE YA SEKONDARI IPELELE,
S.L.P 142,
MAKETE
06/12/2020

KUMB. NA. IPSS/JINS/VOL.1/10

JINA LA MWANAFUNZI

……..

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA 2021 SHULE YA SEKONDARI IPELELE

Ninayo furaha kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga **kidato cha kwanza** katika shule ya **sekondari ipelele mwaka 2021**. Aidha ninachukua fursa hii kukupongeza kwa kufaulu mtihani wako wa **darasa la saba.** Hii ni bahati ya pekee ambayo wachache wameipta, wewe ukiwa ni mmojawapo.

Ni matumaini yangu kuwa utakuwa na nidhamu nzuri na utatekeleza na kufuata sheria na kanuni zote za shule hii ikiwa ni pamoja na masharti yote muhimu ya kuzingatia kwaajili ya kujiunga na shule hii. Shule ya sekondari ipelele ni ya mchanganyiko, pia ni shule ya kutwa kwa wavulana na ya bweni kwa wasichana.

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

1. TAREHE YA KUWASILI SHULENI

Shule itafunguliwa tarehe **11/01/2021**. Unatakiwa kuwepo shuleni kuanzia saa moja na robo asubuhi (**07:00AM**). Endapo hutafika shuleni tarehe tajwa hapo juu hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yako. Unatakiwa kufika shuleni na **mzazi/mlezi** wako ili afanye mambo yafuatayo:

a) Awasilishe mchango wa chakula kama serikali ilivyoagiza pamoja na kamati ya chakula ya shule.
b) Arudishe fomu ya kukubali nafasi hii.
c) Arudishe fomu ya maelezo binafsi yahusuyo mwanafunzi.
d) Arudishe fomu maalumu baada ya kupata vipimo na daktari wa hospitali.

- **VYOTE HIVYO VIWE VIMEJAZWA KWA USAHIHI**

2. VIFAA UNAVYOTAKIWA KUJA NAVYO

a) SARE ZA SHULE (WAVULANA)

i. Shati mbili nyeupe mikono mifupi zenye ukosi (kola).
ii. Suruali mbili za kitambaa cheusi moja na ya damu ya mzee moja (vitambaa hivi vimeambatanishwa kwenye fomu).
iii. Soksi pair mbili rangi ya khaki au nyeupe.
iv. Raba za michezo pair moja.
v. Bukta mbili za michezo.
vi. Sweta rangi ya bluu.
vii. Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba.
viii. Tracksuit ya michezo rangi ya bluu au nyeusi.
ix. Jembe moja na ndoo moja kwaajili ya shughuli za usafi wa mazingira pamoja na uzalishaji mali.
x. Daftari kubwa zisizopungua 10 (COUNTER BOOK).
xi. Mkebe wenye vifaa vyake.
xii. Rula na kalamu ya wino
xiii. Bunda moja la karatasi (rimu)
xiv. Mchango wa mahafali kiasi cha Tsh 5000/=

MCHANGO WA CHAKULA KWAAJILI YA WAVULANA

MAHINDI DEBE 5 @12,000/=	60,000/=
MAHARAGE DEBE 01 @ 40,000/=	40,000/=
MCHELE DEBE 1 @ 40,000/=	40,000/=
KULIPA MPISHI	5000/=
KUKOBOA NA KUSAGA	10,000/=
KUNUNUA SUKARI	10,000/=
VYOMBO VYA KUPIKIA	2000/=
MAFUTA YA KUPIKIA	10,000/=
VIUNGO/MBOGA ZA MAJANI	4000/=
NYAMA	6000/=
JUMLA KUU	**187,000/=**

WASICHANA

i. Blauzi (shati) mbili nyeupe za mikono mifupi staili ya **SOLO** zenye kola.
ii. Suruali mbili moja nyeusi na nyingine ya damu yam zee (kitambaa kimeambatanishwa kwenye fomu hii)
iii. Gauni mbili za kushindia (shamba dress) rangi ya bluu bahari kitmbaa cha satini zenye urefu wa 25 cm gotini mshono wa solo.
iv. Mashuka mawili (02) ya kutandika rangi ya bluu na pinki.
v. Soksi rangi ya khaki au nyeupe.
vi. Raba za michezo pair moja.
vii. Sweta rangi ya bluu.
viii. Bukta mbili za michezo.
ix. Viatu vyeusi vyenye kamba na vyenye visigino vifupi.

x. Ndoo mbili za lita kumi, dish moja, taulo kwaajili ya kuogea.
xi. Godoro dogo la inchi tatu (03) pamoja na blankent.
xii. Tracksuit ya michezo rangi ya bluu au nyeusi.
xiii. Vifaa kwaajili ya kulia chakula pamoja na fedha kwaajili ya matumizi binafsi (pocket money)
xiv. Daftari kubwa zisizopungua kumi (counter book).
xv. Mkebe wenye vifaa vyake.
xvi. Jembe moja kwaajili ya usafi wa mazingira pamoja na uzalishaji mali.
xvii. Bunda moja la karatasi (rimu)
xviii. Mchango wa mahafali (5000/=)

MCHANGO WA CHAKULA KWAAJILI YA WASICHANA (WOTE WATAKAA BWENINI)

MAHINDI DEBE 7 @12,000/=	84,000/=
MAHARAGE DEBE 02 @ 40,000/=	80,000/=
MCHELE DEBE 1 @ 40,000/=	40,000/=
KULIPA MPISHI	5000/=
KUKOBOA NA KUSAGA	10,000/=
KUNUNUA SUKARI	10,000/=
VYOMBO VYA KUPIKIA	2000/=
MAFUTA YA KUPIKIA	10,000/=
VIUNGO/MBOGA ZA MAJANI	4000/=
NYAMA	6000/=
JUMLA KUU	**251,000/=**

- Unaruhusiwa kuleta nafaka kama mchele, mahindi na maharage badala ya kuleta fedha. Kama nafaka huna basi ulete pesa kama zilivyoonyeshwa hapo juu. Waweza lipa mchango kwa mwaka mzima au nusu muhula pia.
- Kabidhi mchango wako kwa kamati ya chakula na si mahala pengine na hakikisha unapewa risiti kwa kila mchango utakaolipia (wajumbe wa kamati ya chakula watakuwepo shuleni hapa kipindi hiki shule inapofungua).
- Mwanafunzi ambaye hataripoti shuleni hatua kali zitachukuliwa dhidi yake, mlezi/mzazi wake.

3. MWISHO

Kwa niaba ya wizara ya elimu pamoja na shule, ninakukaribisha sana. Ni matumaini yangu kuwa utaitumia nafasi hii kwa manufaa yako na ya Taifa kwa ujumla. Tunategemea kuwa utajiepusha na vitendo vyote viovu na kuwa mstari wa mbele katika mambo yote yaliyokuleta shuleni hapa.

……

JOHN AMON
MKUU WA SHULE (0767607881)
SHULE YA SEKONDARI IPELELE